

**MTIHANI WA MWIGO
WA
SUPA JET
KISWAHILI.**

102/2

Karatasi ya 2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha, Isimu Jamii)

Juli / Agosti - 2013.

Kidato Cha 4.

Muda: 2 ½.

Jina.....Nambari.....

Jibu maswali yote.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

	Swali.	Upeo.	Alama.
1	Ufahamu.	15	
2	Ufupisho.	15	
3	Matumizi ya lugha.	40	
4	Isimu Jamii.	10	
JUMLA.		80	

1. UFAHAMU – (Alama 15).

Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali yafuatayo.

Wanawake, wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoenedelea ni baadhi ya watu waliopea na kuboea katika uchochole mkubwa. Jumla ya idadi kubwa ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya million 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu pamoja na kuwako kwa matatizo ya kiuchumi duniani. Kadhalika matatizo mengine na mitafuruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasili mathalani mafuriko, ukame na milipuko ya volcano. Usisahau pia kuwa kuna uharibifu wa kimazingira, mabadiliko ya desturi na kusambaratika kwa familia na misingi yake. Tatizo lingine ni kuwa kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza familia zinazosimamiwa na wanawake (ambao tumewataja kuwa wanakumbwa na umaskini mkubwa.)

Wanawake wanaoishi mashambani wanakumbwa na makubwa. Kwanza, kama maskini wanaishi katika mazingira magumu. Vile vile kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamabaduni yanayowadharau na kuwapuza wanawake na mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa familia, hasa wanaolea na kutunza jamaa za mzazi mmoja, wanapambana na uongozi wa familia pamoja na uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi wowote katika majukumu kama haya bali wanalazimika kupambana nayo peke yao. Kutokana na hayo yote wanawake hawapati nafasi nzuri kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahu. Maswala mengi yanaamuliwa na wanaume pasipo kuwahusisha wanawake.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia mbali mbali. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii, taifa na familia. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa wanawake ndio chanzo cha nguvukazi kwani ni wao na watoto wao wanaotekeleza kazi nyingi hasa za nyumbani na mashambani. Mara nyingi huwa na uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wenzao wanaume.

Kifamilia wanawake wa mashambani wanashugulika mchana kutwa katika hali ngumu ya hewa aidha juu kali au mvua huku wameeleka wanao migongoni wakilima mashamba ili kupata chakula kwa familia zao. Jukumu la kuandaa chakula nyumbani bado linaachiwa wale wale wanawake wanaokizalisha mashambani.

Jambo lisilopingika ni kwamba wanawake wanatekeleza majukumu makubwa na muhimu katika kizazi cha binadamu na ndio hasa mihimili ya jamii yoyote staarabu. Kwa hivyo, ni kinaya kitupu kudhalilisha wanawake. Mataifa mengi yaliyoedelea ni yale yaliyoondoa vikwazo vyote mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao. Kadhalika wanaume wa huko wanawaona wanawake kuwa wenzao katika kujenga jamii wala sio

watumwa au watumuishi wa wanaoumia na kutumikishwa kama vifaa na bidhaa. Inafaa jamii zinzodunisha wanawake zitambue kuwa ubaya wa tendo hili sio tu kudumaza maendeleo yake bali pia kutoa mfano mbaya kwa vijana ambao wataendeleza ukandamizaji huu kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, jamii inawabijika kutenda liio sawa kwa kuwapa hadhi wanawake wote.

Maswali

- (a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (al. 1)

.....
.....

- (b) Nakili maafa matatu ya kimaumbile yaliyotajwa katika kifungu hiki. (al. 3)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

- (c) Eleza sababu tatu zinazowazuia wanawake kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu kulingana na makala haya. (al 3)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

- (d) Wanawake hutekeleza majukumu gani katika jamii na taifa kutokana na makala haya? (al 3)

past papers visit www.ez-learn.com

- (e) Kuna tofauti gani baina ya wanawake wa mataifa yaliyoendelea na yale ambayo hayajastawi. (al 2)

- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyo tumiwa kwenye taarifa. (al 3)

- (i) uchochole

.....

- (ii) kudhalilisha

.....

- (iii) mitafuruiku

.....

2. UFUPISHO – (Alama 15).

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Dawa za kulevyta zinaweza kugawika katika makundi mawili makuu: dawa hasi na dawa sugu. Katika kundi la kwanza zinaingia dawa zozote ambazo hunywewa, kunuswa au hutumiwa kwa nia ya kulevyta au kumwingiza mtumiaji katika hali ya kujihisi amepanda'. Dawa za aina hii huwa na matokeo hasi kwenye mwili wa mtumiaji. Inawezekana jamii ikakubali kuwepo kwake, pamoja na kutumiwa kwake, lakini, matumizi ya kipindi kirefu huwa na matokeo mabaya sana kwa watumiaji. Baadhi ya dawa hizi ni bidhaa za tumbaku ambazo huwa na aina za kemikali inayoitwa nikotini. Nyingine ni vimeo kama wiski, bia, divai, miraa au mairungi, gundi ya viatu na bidhaa zinazotokana na petroli.

Hebu sasa tuangalie zile zinazoitwa dawa sugu. Hizi ni dawa ambazo Kimsingi humchangamsha mtumiaji na kumfanya apandwe na nishati za ajabu. Dawa hizi hufanya hivi kwa kuzitekenya seli za ubongo wa anayehusika. Katika kulifanya hili dawa zenyewe huishia kuzuia seli za ubongo huo. Huu ndio msingi wa mtumiaji kuwa na ustahimilivu fulani wa dawa zenyewe. Ustahimilivu huu ndio unaomfanya awe kama aliyetawaliwa na dawa hizo. Yaani mtumiaji huwa hana njia nyingine ya kujizuia na huishia kuwa mtumwa wa dawa hizo. Baadhi ya dawa sugu ni bangi, afyuni, heroini, mihadarati na kokeini. Baadhi ya wataalamu wanajumlisha miraa katika kundi hili pia. Ni kawaida kusikia madai kuwa mtu anayetumia dawa za kulevyta huonekana kuwa na furaha kuliko wenzake. Ili kuelewa chanzo cha msisimko na furaha hiyo ya ajabu, lazima tuzijue hatua anazopitia mtumiaji dawa za kulevyta. Kimsingi kuna hatua tatu kuu. Mara tu mtu anapozitumia dawa za kulevyta, dawa hizo huzichangamsha seli za ubongo kwa kiasi kikubwa. Kuchangamshwa huku kwa seli kunazuia mwili wa anayehusika kutopata hisia kutoka viungo vya mwili au misuli ya mwili. Matokeo ya hali hii ni kumfanya mtu anayehusika kutenda mambo kupita kawaida yake. Mathalan, ataonekana kuwa na furaha nyingi, atasoma kupita kawaida, anaweza kucheza kwa kipindi kirefu na kadhalika. Hali hii inaweza kuitwa hali ya 'mpumbazo.' Mpumbazo huu unaweza kumdanganya anayehusika kuhisi kuwa ana uwezo usiokuwa wa kawaida. Lakini hii ni hali ya muda tu ambayo hutangulia kuuliwa na kuharibiwa kwa seli za ubongo.

Mtumiaji anayeingia katika hatua ya pili huwa anatoka kwenye ile hali ya mpumbazo. Hatua ya pili hutambulishwa na dalili zifuatazo: Uchovu, kulala kupita kiasi, kutokuwa na hamu ya kazi au mambo mengine. Kupuuza maswala ya siha na afya, usahafuli, kukosa malengo au shabaha katika kazi yake, kupungukuwa na kumbukumbu, kujitenga na watu wengine na kuwa na hisia za chuki au uhasama na jamaa. Mtumiaji anapofikia hatua hii hutambulikana waziwazi na watu walio karibu. Mtumiaji wa dawa za kulevyta huweza tu kunusurika au kuokolewa katika hatua hii. Akipita hatua hii ya pili, huwa anaingia katika awamu mbaya sana.

Hatua ya tatu ya mtumiaji wa dawa za kulevyta huitwa hatua 'isiyo ya kawaida.' Sifa za kutambulisha mtumiaji aliye kwenye ngazi hii ni fadhaa kubwa, unyonge wa mwili uiimbu wa kimawazo na uvunjifu mkubwa. Mtumiaji aliyefikia ngazi hii huonyesha sifa kadha milele. Mathalani kujitenga kabisa na jamaa au watu walio karibu naye, kupaliwa kabisa na usingizi, kuudhika haraka na kuwa na tabia ya kuonyesha uchukivu wa vitu kwa kupigana, kuchanganyikiwa kunakotokana na kuharibikiwa kwa seli za ubongo, wazimu au kuangukaanguka kama mgonjwa wa kifafa. Katika ngazi hii, seli za ubongo

~~zina~~ zinazomsaidia mtu kufanya uamuzi mzuri huwa zimeharibiwa na dawa zenyewe. Si ajabu basi kuwa mtumiaji anaonyesha tabia za kitoto na huishi kama mtu aliye kwenye ndoto. Hatimaye ubongo unazonongwa kabisa kutokana na madhara ya seli na mtumiaji huweza kushikwa na magonjwa ya kiakili kama wendawazimu.

Mwisho wa mtumiaji ~~wala~~ dawa za kulevya aliyefikia ngazi hii ni kufariki baada ya mwili wake kushindwa ~~kuhimili~~ uzito wa dawa zenyewe. Wengine huishia kujinyonga au kufariki kutokana na madhara ya moyo.

Maswali.

- a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili.
~~maneno 45 - 50~~
Matayarisho (al 7)

Nakala safi

- b) Eleza hatua anazopitia mtumiaji wa dawa za kulevya.
(Maneno 90 - 100)
Matayarisho (al 8)

Nakala safi

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

3. MATUMIZI YA LUGHA - (Alama - 40).

- a) Eleza njia mbili za kuainisha konsonanti. (al 2)

(i)

.....

.....

(ii)

.....

.....

- b) (i) Fafanua maana ya kishazi tegemezi. (al 1)

.....

.....

- (ii) Huku ukitoa mifano, elezo sifa mbili za vishazi tegemezi. (al 2)

.....
.....
.....
.....
.....

- c) Sahihisha sentensi hii. (al 2)

Mwanafunzi mwenye alipigwa na kiboko juu ya kutokamilisha kazi alisirai.

.....
.....
.....

- d) Andika katika msemo wa taarifa. (al 3)

“Nimeonewa,” mshtakiwa alilalamika, “sijashiriki ulevi tangu mwaka jana!”

.....
.....
.....

- e) Tunga sentensi mbili kubainisha matumizi ya vitate hivi. (al 2)

- (i) Fuja
(ii) Vuja

.....
.....
.....
.....
.....
.....

- f) Andika neno hili katika ufupi. (al 1)

Shangazi zako

.....
.....

- g) Tunga sentensi ukitumia neno na kama kihuishi cha mtendaji. (al 1)

.....
.....
.....

- h) Changanya ukitumia visanduku. (al 4)

Anita Mwendwa na Olisa wamekuwa wakilima shamba lililopandwa mahindi.

- i) Tumia kitenzi kisaidizi katika sentensi hii kinachoonyesha uwezekano. (al 2)

Jua litawaka sana leo.

.....
.....
.....
.....
.....

- j) Eleza miundo ya silabi za neno lifuatalo. (al 3)

Dhaifu

- k) Andika vitenzi vinavyotokana na nomino zifuatazo: (al 2)

- (i) Mtihani
(ii) Sitara

I) Virai vilivyopigiwa mstari ni vya aina gani? (al 2)

(i) Shujaa Nelson Mandela ni mgonjwa.

.....
.....

(ii) Hivi karibuni shule iliyofungwa itafunguliwa.

.....
.....

m) Badilisha shamirisho kipozi katika sentensi ifuatayo iwe shamirisho kitondo. (al 2)

Rispa alipigwa na mama.

.....
.....

n) Neno muundi liko katika ngeli gani? (al1)

.....

o) Andika katika wingi. (al 1)

Petroli iliyonunuliwa na dereva huyo imemwagwa.

.....
.....
.....

p) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:- (al 3)
Hakijanunulika

.....
.....
.....
.....
.....
.....

q) Eleza hali katika sentensi zifuatazo:- (al 1)

(i) Anasimama akaimbe.

.....
.....
.....

- (ii) Wakulima wapanda ngano. (al 1)

.....
.....
.....

- r) Huku ukidhibi mirisha maana mbili tofauti, tia shadda katika neno lifuatalo. (al 2)

Walakini

- s) Tunga sentensi moja yenyе chagizo ya idadi. (al 1)

.....
.....

- t) Kamilisha sentensi kwa mnyambuliko sahihi wa kitenzi –pa.

Nyambura na Fiona _____ salamu walipokutana. (al 1)

4. ISIMU JAMII – (Alama 10).

Mtu I : Wapi kitambulisho?

Mtu II : Nimesahau nyumbani Afande.

Mtu | : Afisaat Ingiza hii jambazi ndani. Anachezea nani akili!

Mtu | : Na wewe? Unataka nini hapa?

Mtu II : Sir. majambazi wameniyamia nijani

- a) (i) Hii n̄sajili gani? (al 1)

1st

- (ii) Eleza sifa nne za sajili uliyotaja hapo juu. (al 4)

.....

.....

.....

.....

[View Details](#) | [Edit](#) | [Delete](#)

.....

.....

- b) Fafanua namna Kiswahili kilivyoenezwa katika kipindi kabla ya Uhuru barani Afrika. (al 5)

.....

.....

.....

.....

.....